# LEARNING BY EAR

## Lent Luxury - The risks of raising credit

## EPISODE FOUR: THE OPERATIONAL RISK

**AUTHOR: James Muhando**

**EDITORS: Adrian Kriesch, Friederike Müller**

**PROOFREADER: Tony Dunham, Pendo Paul**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

**LIST OF CHARACTERS BY SCENE.**

**SCENE ONE: AT GIDDY'S.**

- **GIDDY( M 15)**
- **JENNY(F 15)**
- **JD(M 15)**
- **NARRATOR( M 30)**

**SCENE TWO: IN THE BANK**

- **UNCLE BARRY(M 45)**
- **CUSTOMER CARE OFFICER( F MID 20'S)**
- **MR.GEORGE MANDO(M 45)**
- **NARRATOR(M 30)**

**SCENE THREE: AT GIDDY’S.**

- **GIDDY(M 15)**
- **LUCIA (F 11)**
- **NARRATOR(M 30)**

**SCENE FOUR: AT SUZIE’S AUTO SPARE SHOP.**

- **NARRATOR(M 30)**
- **SUZIE( F 40’S)**
- **LUKA(M 45)**
- **SHOP ASSISTANT(M/F ADULT)**

**SCENE FIVE: IN CLASS.**

- **NARRATOR(M 30)**
- **JD(M 15)**
- **LUKA(M 40’S)**
- **5 - 8 STUDENTS (around 15 years)**

**INTRO:**

**1. SFX: OFFICE AMBIENCE**

**2. SFX: FAN SWITCHED ON**

**3. NARRATOR:**

(Yawns) Karibu kwa sehemu hii ya nne ya mfululizo wa vipindi vya Noa Bongo Jenga Maisha yako kuhusu Mchezo huu wa Redio 'Starehe za Kuazima' –Tatizo la kulipa Mkopo". Jina langu ni Gideon Leboo, afisa anayehusika na masuala ya mikopo katika benki hii ya Jubilee, na pia mhusika mkuu katika mfululizo wa vipindi hivi. Samahani nimechoka kidogo leo kwa sababu mara nyingine ofisi yangu huwa na shughuli nyingi sana! Kidogo nilikuwa nimeanza kusinzia! Kwa hakika lazima wafikirie kuweka kiyoyozi hapa ofisini! Nafikiri ndio sababu ya kila mara nakumbuka enzi za ujana wangu.! (**laughs**)

Katika kipindi kilichotangulia nilimueleza jinsi rafiki yangu JD alifunzwa adabu na mamake kwa kudanganya kwamba amekuwa akihudhuria shule kumbe wapi! Ukiwa tumeketi kando kando ya mto, Mimi ,Jenny, JD , tulizungumza kwa kirefu tatizo lililomkuta JD kuhusu baiskeli yake, aliyoichukua kwa mkopo. Kwa hakika, halikuwa jambo la busara kukopa pesa kutoka kwa Gori! Alitaka dhamana ya mkopo huo endapo tutashindwa kuulipa. Kisha wazo jingine la kipuuzi likanijia.

**SCENE ONE: AT GIDDY’S.**

4. **SFX:** **DOOR OPENS, FOOTSTEPS, THREE PEOPLE INTERIOR**

5. **GIDDY:** **(Whispering)** Shh! Kuanzia sasa tunapaswa kuwa waangalifu zaidi. Tunanyanyapaa! Na kuongea kwa sauti ya chini zaidi! Tumeelewana?

6. **JENNY:** **(Whispering)** Lakini hujatuambia tunafanya nini hapa nyumbani kwenu! Kwanini tunajifichaficha?

7. **GIDDY:** Nimekwambia kuwa na imani mambo yatakuwa sawa.. Tunachukua Redio ya Mjomba Barry kwenda kuiweka dha..dhamana... kule kwa Gori...

8. **JD:** Dhamanal, Wewe!

9. **JENNY:** **(Shocked)** Samahani? Kwani tunaiba redio ya mjombako ili kupata mkopo kutoka kwa yule Mzee?

10. **GIDDY:** Shh! Zungumza kwa sauti ya chini! Tunachukua, sio kuiba..Jenny!

11. **JENNY:** Vyovyote vile! Na utamwambia nini mamako?

**12. GIDDY:** Usiwe na wasi wasi! Hatajua kinachoendelea! Hii redio imekuwa ikilala hapa chumbani kwangu kwa muda mrefu sana! Huwa hatuitumii, na mjomba Barry hajaonekana nyumbani kwa muda wa miaka miwili sasa! Lazima tupate mkopo kutoka kwa Gori. Baadaye tutakwenda kuikomba na kuirudisha chumbani bila ya mtu yoyote kujua!

**13. SFX:** **DOOR OPENS.**

**14. GIDDY:** Ile pale kwenye boksi juu ya kabati! ....JD, nisaidie. Nisaidie!

**15. JD :** **GRUNTS AS HE HOISTS HIM UP**

**16. SFX:** **CARTON PULLED FROM CUPBOARD, PUT ON SURFACE**

**17. GIDDY:** **(Pants)** Tutaitoa kwenye boksi kisha turudishe boksi hilo juu ya kabati ili mtu asishuku chochote.

**18. JD :** **GRUNTS AS HE HOISTS HIM UP AGAIN**

**19. SFX:** **CARTON PUSHED BACK ON THE CUPBOARD**

**20. GIDDY:** Sasa twendeni!

**21. SFX:** **3 FOOTSTEPS LEAVING**

**22. NARRATOR:**

Sote tumefurahi sasa!. Kwa kufanya hivyo tulidhani ni werevu! Lakini kumbe hatukujua kwamba kunawerevu zaidi yetu! Dadangu mdogo, Lucia! Alisikia na kuona yote yaliyokuwa yakiendelea. Alikuwa amejificha chini ya kitanda changu. Na sijui kwanini sikufikiria kuchungulia chini ya kitanda kama kawaida yangu!

Wakati huo huo, mjombangu Barry ambaye anaishi jijini alkuwa akielekea Benki.

**<u>SCENE TWO: IN THE BANK.</u>**

**23. ATMO: BANK HALL AMBIENCE**

**24. UNCLE BARRY:** Samahani!

**25. CUSTOMER CARE OFFICER:** Bila ya samahani, naweza kukusaidia?

**26. BARRY:** Nimekuja kumuona Bw. Mando!

***KW begin***

**27. CC OFFICER:** Subiri kidogo tafadhali!

**28. SFX: DIALS PHONE**

**29. CC OFFICER:** Hallo, Bw. Mando. Kuna mtu anataka kukuona hapa. ..samahani…. **(To Barry)** Jina lako?

30. **BARRY:** Barnabas Leboo!

31. **CC OFFICER: (On phone)** Barnabas Leboo. Sawa..!

32. **SFX: MOUTH PIECE PLACED BACK**

***KW end***

33. **CC OFFICER:** Pita ule mlango, kisha pinda kushoto, atamuona.

34. **BARRY:** Asante!

35. **SFX: FOOTSTEPS, DOOR OPENS AND CLOSES**

36. **MR. MANDO: (Happily)** Barnabas Leboo! Habari yako?

37. **BARRY:** Njema, Bw. Mando!

38. **MR.MANDO:** Ehh ni muda mrefu sana,... tangu lini vile? Tumekuwa marafiki wakubwa sana shuleni!

39. **BARRY:** Kweli, hadi uliposafiri ng'ambo kwa masomo zaidi ndipo ukanisahau kabisa!

40. **MR. MANDO: (Laughs)** Siwezi kukusahau! Uliniambia wewe ni mwekezaji katika sekta ya yumba?

41. **BARRY:** Ndio..! Na ndio sababu niko hapa. Nahitaji pesa. Moja kati ya miradi yangu imekwama.

42. **MR.MANDO:** Kwa hiyo unakata mkopo wa benki .. au..?

43. **BARRY:** Hata ikiwa ni mkopo kutoka kwa wewe rafiki yangu,.. au popote pale!

44. **MR.MANDO:** Nitakujulisha kwa meneja wetu.

45. **BARRY:** Subiri kwanza ! Nataka unielewe kwamba sina dhamana yoyote.

46. **MR.MANDO:** Unahitaji kiasi gani?

47. **BARRY:** Dola 1,400, kiasi cha pesa zitakazonisaidia hadi pale mambo yangu yatakapoimarika tena!

48. **MR.MANDO:** Utalipa lini?

49. **BARRY:** Baada ya mwezi mmoja hivi!

50. **MR.MANDO:** Sawa , mimi nitakukopesha pesa zangu, bora tu una ahidi kunilipa siku tutakayokubaliana. Lakini naweza kukukopesha dola 400 pekee!

51. **BARRY:** Nashukuru sana! Asante! Sitakosa kutimiza ahadi hiyo.

52. **NARRATOR:**

Maskini Bw. Mando. Ametapeliwa! Kwani huu ndio uliokuwa mwisho wa kumuona mjomba Barry. Sisi watu wa benki tunasema *defaulted, yaani Mtu anaposhindwa kulipa deni !*

Nilipokuwa nikirejea nyumbani baada ya kupata pesa tulizohitaji kutoka kwa Gori kwa kutumia Redio ya Mjomba Gori kama dhamana, kwa hakika nilisikia furaha isiyo na kifani kwa kuwa nilikuwa nimeweza

kumsadia rafiki yangu JD. Hata hivyo, lakini sikuwa na habari yaliyokuwa yakinisuburi chumbani kwangu.

**SCENE THREE: AT GIDDY'S**

**53. SFX:** **FOOTSTEPS INSIDE APPROACH, DOOR OPENS.**

**54. GIDDY:** **(Whistles as he opens door).**

**55. LUCIA:** **(Suddenly)** Boo-hoo!

**56. GIDDY:** **(Screams startled)** Lucia! Umenishtua!

**57. LUCIA:** **(Laughs, sings as she claps)** Pongezi, pongezi sana Giddy! Umeng'ara kama nyota!

**58. GIDDY:** Toka chumbani kwangu, Lucia!

**59. LUCIA:** Nimekuona! Nikwambie umefanya nini!

**60. GIDDY:** **(Not amused)** Nimefanya nini?

**61. LUCIA:** Nimekuona na rafiki zako mkiiba redio ya mjomba Barry!

**62. GIDDY:** **(Alarmed)** Lucia, tafadhali usiniseme. Nitafanya chochote unachotaka!

**63. LUCIA:** Chochote?

**64. GIDDY:** Chochote unachotaka!

**65. LUCIA:** Utafanya kazi zangu za shule?

**66. GIDDY:** Ndio!

**67. LUCIA:** Na kufagia nyumba?

**68. GIDDY:** Hakuna shida kabisa! Ilimradi usiniseme.

**69. LUCIA:** Na... pia utaosha vyombo wiki ijayo!

**70. GIDDY:** Tafadhali nitafanya chochote lakini sio kuosha vyombo!

**71. LUCIA:** **(Pretends to call the mother)** Mama ! Giddy amei....

**72. GIDDY:** **(Cuts in)** Sawa! sawa! Nitaosha vyombo!.

**73. LUCIA:** **(Laughs) E**ehhe, nimekupata! Kwanza mama hajafika nyumbani bado!

**74. NARRATOR:**

Lakini si mimi pekee niliyekuwa mashakani, JD alikuwa anashindwa hata kufanya kazi zake za kawaida, kwani daima aliandamwa na masaibu kuhusiana na baiskeli yake. Si nyumbani, si shuleni, kila mahali! Na kisha mambo yakabadilika punde babake alipokwenda dukani kwa Suzie kununua vipuri.

**<u>SCENE FOUR: AT SUZIE’S AUTO SPARE SHOP.</u>**

**75. SFX:** **AUTO SPARES SHOP ATMO.**

***KW begin***

**76. SUZIE:** **(Shouts)** John!

**77. SHOP ASSISTANT:** Ndio Mama!

**78. SUZIE:** Tuna *fanbelts* za gari aina ya Volkswagen?

**79. S.ASSISTANT:** Ndio!

**80. SUZIE:** Hebu mletee mteja wangu hapa!

**81. S.ASSISTANT:** Sawa mama!

**82. SFX:** **FOOTSTEPS APPROACHING.**

***KW end***

**83. LUKA:** Habari ya asubuhi mama!

**84. SUZIE:** Nzuri Luka! Habari yako! Na umekuwa wapi siku zote hizi? Biashara yangu itaporomoka ikiwa wateja wangu watanitoroka!

**85. LUKA/SUZIE: THEY LAUGH.**

**86. SUZIE:** Ni kuuzie nini leo?

**87. LUKA:** Nahitaji vipuri kadhaa kujaza karakana yangu. Lakini sina pesa kwa wakati huu!

**88. SUZIE:** Luka unajua mimi sikopeshi. Lakini mimi sina tatizo na wewe maana huwa unalipa!

**89. SFX:** **THEY LAUGH.**

**90. LUKA:** Lakini ni kitambo sana tangu nichukue vitu kwa deni hapa kwako.

**91. SUZIE:** Ni kweli mbali na ile baiskeli uliyomtuma mtoto wako, wiki mbili zilizopita. Si uliichukua kwa mkopo sivyo?

Tuache hayo ya zamani! Kwanza ni vizuri umemaliza kulilipa deni hilo. Ulikuwa unataka nini?

**92. LUKA:** **(Confused)** Hebu ngoja kidogo…Unasema nini? Baiskeli gani?

**93. SUZIE:** Ile ya BMX uliyomtuma mtoto wako JD! Kwanza hata nimeiona ile karatasi barua uliyomtuma mtoto wako. Nilikuwa nataka kuitupa kwa vile tayari ulikuwa umemaliza kulipa.

**94. LUKA:** Samahani. Unasema nini Suzie? Karatasi gani?

**95. SFX:** **PAPER**

**96. SUZIE:** Si hii hapa.

**97. LUKA:** **(Reads aloud)** Suzie, tafadhali mpe huyu mtoto wangu baiskeli . Nitakulipa pesa zilizosalia baadaye. Sahihi, Luka Mwamba**. (To Suzie )** Na hii ulipewa na mtoto wangu JD?

**98. SUZIE:** Kwani si wewe uliandika hii barua?

**99. LUKA:** Hapana! Huyu mtoto amekuwa mkora! Subiri nitamfunza adabu!

**100. SUZIE:** Utamfanya nini? Hata hivyo tayari amelipa!

**101. LUKA:** Haijalishi amelipa au la! Tatizo ni kwamba anataka kuwa tapeli. Nitakuona baadaye!

**102. SFX:** **FOOTSTEPS LEAVE**

**103. SUZIE:** **(Calls)** Na hivi vipuri...! Mali yako unaiacha?

**104. NARRATOR:**

Lakini tayari babake JD alikuwa ameondoka huku akiwa amechanganyikiwa! Wakati huo huo, sisi bado tuko darasani wakati wa mchana tukiwa tumechoka baada ya somo la hesebu. JD amerudi shuleni pia. Mwalimu wa somo linalofuatia bado hajaingia darasani na hivyo tunapiga gumzo tu, mara ghafla....

**SCENE FIVE: IN CLASS.**

**105. SFX: CLASS NOISE**

**106. SFX: DOOR BURSTS OPEN, FOOTSTEPS APPROACH**

**107. LUKA:** JD! Njoo hapa, mjinga wewe! Umenza kuwa tapeli?

**108. JD:** **(Screams)** Aww! Unaniumiza masikio yangu!

**109. LUKA:** Kwanini umeigiza sahihi yangu na kisha kwenda kunidanganya na kuchukua baiskeli?

**110. SFX: COMMOTION AS HE IS DRAGGED AWAY.**

**111. PAUSE (SILENCE)**

**OUTRO:**

**112. SFX: OFFICE AMBIENCE, FAN STILL RUNNING.**

**113. NARRATOR:**

Kimya kilitanda darasani na ungeweza hata kusikia sindano ikianguka sakafuni! Wanafunzi ambao kwa kawaida huwa na kelele sana wakizungumza na kucheka wakati kama huu, sasa walikuwa wamefunga midogo. Badala ya kufanya mambo kuwa magumu angemueleza ukweli Babake au Suzzie! Katika taaluma yangu kama afisa wa benki, ukiwa na deni ambalo huwezi kulilipa, ni vyema uzungumze na yule kiongozi au mwenye deni. Mara nyingi muda wa kulipa deni hilo unaweza kuongeza au hata kufutiliwa mbali.

Basi msikilizaji sasa ni wakati wa kurudi kazini. Ukipenda kusikiliza tena kipindi hiki tembelea mtandao wetu wa dw.de/lbe. Hadi wakati mwengine, kwaheri kwa sasa!